# GUNDUA SHAUKU YAKO

MADA YA

2

***Alama ya Chapisho***

Februari 2022

Programu ya 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' linaweza kuwa huru kutumika, kwa vile chanzo kimetajwa.

***Ilianzishwa na:*** Wil Bom, VSO, mradi wa Vijana na Ajira, Zanzibar, Tanzania

***Kwa ushirikiano na:*** Walimu na wakufunzi wasaidizi wa makundi manne ya Mafunzo ya Ufundi (Amali), Unguja na Pemba; Sophie Oonk wa Randstad Uholanzi ambaye aliendeleza mada ya 5 'Gundua biashara yako'; Kitty den Boogert, rafiki na mwenzangu wa zamani, ambaye aliangalia toleo la mwisho.

***Kwa kuzingatia:*** Warsha (ya mafunzo) ya maendeleo ya kazi, iliyotolewa wakati wa maonesho ya Zanzi Job ya mwaka 2015 na 2016.

Utangulizi wa VSO-ICS juu ya uajiri na ujuzi wa maendeleo ya kazi katika mwaka 2015 na warsha (za mafunzo) zilizotolewa na Watu wenye Kujitolea wa Huduma za Wananchi, Kimataifa.

Mwongozo wa mafunzo, Elimu ya Ujasiriamali na Mafunzo ya EET, Kuboresha Uwezeshaji wa Kiujasiriamali, Moduli ya 1 na 2, VETA, 2014 – 2008.

Maendeleo ya programu kwa mwongozo wa kazi katika mafunzo ya ufundi na CINOP, Uholanzi. www.cinop.nl

Loopbaanmagazijn (Hifadhi ya kazi), ilianzishwa na Claudine Hogenboom, mradi wa Mwongozo wa Kazi kwa mafunzo ya ufundi, Uholanzi. http://www.expertisepuntlob.nl/

Het lespakket netwerken (Mtandao wa Mtaala), ilianzishwa na La Red B.V., Uholanzi. http://lared.nl/

***Tafsiri ya Kiswahili:*** Abdalla Baruan, Dar es Salaam, abbybaruan@gmail.com
Abraham Mtongole, Dodoma, abmtongole@gmail.com
Yahya Abdu, Pemba, Tafsiri ya kiswahili na uhakiki wa toleo la mwisho, yahyarashid@live.com

***Ubunifu:*** Katie Wolgemuth, VSO Dar es Salaam na wanafunzi wa GLU, Grafisch Lyceum Utrecht

***Ilichapishwa na:*** VSO Tanzania, S.L.P 6297, Dar es Salaam Tanzania

***Eneo:*** Ploti na. 997 Msasani, Barabara ya Chole, Dar es Salaam Tanzania

***Simu:*** (+255) 222600072 au (+255) 222600087

***Barua pepe:*** vsotanzania@vsoint.org

***Tovuti:*** www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet




# MAENDELEO YA KAZI NAMNA YA KUWAONGOZA VIJANA KWENYE MAFUNZO YA UFUNDI NA AJIRA AU AJIRA BINAFSI?

## MADA YA 2 GUNDUA SHAUKU YAKO



# YALIYOMO

Kitabu hiki 'Gundua shauku yako' ina vifaa kwa ajili ya mada ya 2 ya programu kwenye Maendeleo ya Kazi. Kwanza, unakuta utangulizi wa jumla kwenye programu na namna ya kuandaa mafunzo. Hii inafuatiwa na maelezo mahsusi ya jumla ya mazoezi ya mada ya 2, maelekezo tofauti kwa kila zoezi na karatasi za mazoezi.


Utangulizi wa jumla Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi naa jira au ajira binafsi 6 - 11

Mada ya 2 na maelezo ya jumla ya mazoezi 'Gundua shauku yako' 12 - 15

TMada ya 2: mazoezi 2.1 - 2.14 16 - 43

Karatasi za mazoezi 44 - 67


Vichwa vya vitabu vyote sita vya programu ya Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi? ni:

1 Gundua kipaji chako
2 Gundua shauku yako
3 Gundua ulimwengu wako wa kazi
4 Gundua mtandao wako
5 Gundua biashara yako
6 Mpango kazi wako na kuomba kazi

Uwasilishaji wa pawapointi na karatasi za mazoezi zinaweza kupakuliwa kutoka www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet

# UTANGULIZI WA JUMLA

# MAENDELEO YA KAZI: NAMNA YA KUWAONGOZA VIJANA KWENYE MAFUNZO YA UFUNDI NA AJIRA AU AJIRA BINAFSI?

**Mradi wa VNA na programu ya 'Ulimwengu Wangu wa Kazi'**
Vijana na Ajira (VNA), mradi wa Vijana na Ajira ni moja ya miradi ya VSO, Volunteer Services Oversee (Huduma za Kujitolea, Ng'ambo) kwa ushirikiano na RGZ, (Revolutionary Government of Zanzibar/Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar). Moja ya vipengele vya mradi wa VNA ni programu ya 'Ulimwengu Wangu wa Kazi' (UWwK).

Programu ya UWwK hutaka kuimarisha nafasi ya kijamii na kiuchumi ya vijana ndani ya Zanzibar kwa kuendeleza ustadi mbalimbali wanaouhitaji kwa ajili ya ajira, ajira binafsi au ujasiriamali. Kwa kusudio hilo, viunganishi madhubuti zaidi baina ya sekta binafsi na mafunzo ya ufundi ni muhimu. Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi (Amali) (MMA), NACTE (Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi), Vituo vyote vya Mafunzo ya Ufundi (Amali) na Taasisi za Zanzibar zinahusishwa kama washirika katika programu hii ya UWwk. Wana majukumu makubwa katika kuwawezesha vijana pamoja na ujuzi muhimu kuingia katika soko la ajira.


Programu ya UWwK imezalisha sanduku la zana kwa masomo mawili ya msingi: Mafunzo na Elimu ya Kuzingatia Umahiri na Maendeleo ya Kazi. Unaweza kupata sanduku zima la zana kwenye mtandao: www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet

**Maendeleo ya Kazi**
Programu ya 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' ikiwemo uchaguzi mpana wa mazoezi ya darasani ambayo husaidia wanafunzi, watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi kupata kuonekana zaidi katika mazingira ya kazi. Kwa kufanya kazi, wote, wale wa ndani ya darasa na nje katika mazingira halisi, vijana hupata habari za hapo kwa hapo kuhusu ulimwengu wa kazi, hufanya kwa vitendo ujuzi tofauti wanaouhitaji kwa ajili ya maendeleo yao ya kazi na hubadilishana uzoefu kwa kila mmoja kati yao. Vipindi vitabuniwa na kutolewa na VMA (Vituo vya Mafunzo ya Amali), Taasisi za Ufundi, Skuli za Sekondari na mashirika mengine ya kiserikali na yasio ya kiserikali, kawaida ni kwa mchango wa wafanya biashara wa ndani (wenyeji). Waajiri na kiongozi (meneja) wa rasilimali watu anaweza kuwa msaada kwa kuwezesha safari za kimasomo, kwa kuwa mkufunzi mgeni wa ndani ya madarasa au kwa kutoa mafunzo ya viwandani.

**Programu ya Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?**

Programu ya Maendeleo ya Kazi huwawezesha walimu wa skuli za sekondari, wakufunzi wa taasisi za mafunzo ya ufundi, kampuni, taasisi zisizo za kirerikali, wizara ya Kazi, Ajira, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Amali) kuchagua mazoezi ambayo yanafaa kwa mahitaji na kiwango cha makundi yao ya vijana.

Programu hailengi kwa vijana kufanyia kazi kwa kujitegemea, bila mwongozo wowote. Bila shaka, washiriki hupata kazi au kazi fulani ya kufanya mmoja mmoja, lakini kwa jumla, hii ni programu ambayo inahitaji mwingiliano, ushirikiano katika makundi na mrejesho. Haiwezi kufuatwa bila mwongozo. Hakikisha unatoa daftari ambalo washiriki wanaweza kuandika na kuhifadhi matokeo na maendeleo yao. Kwenye gamba la daftari, unaweza kuweka mwelekeo wa kazi au washiriki wanaweza kubuni ukurasa wao wa mbele. Walimu na wakufunzi wanahitaji kujiandaa vizuri, na inapendekezwa kwamba mwanzo watafakari maendeleo yao wenyewe ya kazi. Kwa njia hii, walimu na wakufunzi pia ni mfano wa kuigwa katika kuendesha kazi yao wenyewe kiundani.




**Mahiri sita za kazi na dira ya kazi**

Programu 'Maendeleo ya Kazi: namna ya kuwaongoza vijana kwenye mafunzo ya ufundi na ajira au ajira binafsi?' imeundwa karibu na mahiri sita ambazo ni muhimu wakati unapotaka kuendeleza kazi yako:

1 Gundua kipaji chako: tafakuri kuhusu uwezo, kupitia umahiri wako mwenyewe kwa heshma ya kazi yako;

2 Gundua shauku yako: tafakuri kuhusu hamasa, kupitia matakwa na maadili yako mwenyewe kwa heshima ya kazi yako;

3 Gundua ulimwengu wako wa kazi: utafutaji wa ajira, mwelekeo kuhusu maadili na umahiri wako kulinganisha na kinachohitajika katika hali ya kazi za kitaaluma;

4 Gundua mtandao wako: mtandao, kufanya na kudumisha mawasiliano ambayo ni muhimu kwa kazi yako;

5 Gundua biashara yako: utafutaji wa ajira binafsi, mwelekeo juu ya matarajio na umahiri wako kuanza biashara au kuendeleza kazi kama mjasiriamali;

6 Mpango kazi wako na kuomba kazi: udhibiti wa kazi, mipango inayohusiana na kazi na ufafanuzi binafsi wa nafasi kwa mchakato wako wa kujifunza na kazi.

Kila umahiri wa kazi umeshikamanishwa sambamba na swala la kazi na jumla ya mahiri sita zinawakilishwa kama usukani wa uendeshaji wa kazi. Unahitaji kuendesha hatua zako za kazi muda wote kutafuta mwelekeo sahihi. Katika maelezo ya kina ya kila moja ya mahiri sita za kazi, unaweza kupata ufafanuzi zaidi kuhusu umahiri unaouhitaji kufanya kwa vitendo, kuendeleza kazi.

**Namna ya kutumia programu kwenye Maendeleo ya Kazi?**
Kila umahiri wa kazi unaweza kufunzwa kwa kufanya mazoezi kadhaa. Mazoezi hutofautiana katika maudhui na katika mbinu pia. Hii ni nzuri, kwa kuwa kuna njia zaidi ya moja ya kujifunza umahiri wa kazi.

Mwanzoni mwa kila mada mpya, utakuta maelezo ya jumla ya mazoezi yote ambayo ni ya mada maalum. Katika maelezo hayo ya jumla, kawaida unakuta: jina (kichwa) cha zoezi, lengo na muhtasari wa mbinu chochezi ambazo zinaweza kutumika katika zoezi hili. Kwa njia hii, unaweza kuangalia kwa haraka mazoezi yote na hii itakusaidia kufanya uchaguzi unaokufaa na kundi lako. Uchaguzi mzuri ni ule unaohusiana na maswala ya maendeleo ya kazi ambao wanafunzi, watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi wanao.

Baada ya kuchunguza maelezo ya jumla, unaweza kuvuta mazoezi uliyochangua. Yote kati yao yana muundo sawa. Kwa njia hii, unaweza kuona kwa urahisi namna ya kuandaa na kutoa zoezi kwa njia inayofaa.

Kwa kufanya uteuzi wako mwenyewe, walimu na wakufunzi wanaweza kubuni programu ya mafunzo. Unachagua mazoezi yale ambayo yanafaa kwa mtaala, ratiba ya vipindi vya kozi na kiwango cha wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi. Uchaguzi unaofanya pia hutegemea na maswali ambayo wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi wanayo kuhusu kazi yao.

Walimu na wakufunzi wanaweza pia kuchagua yale mazoezi wanayopenda kusomeshea. Baadhi ya mazoezi na mbinu zitakufaa zaidi kuliko nyengine. Vidokezo vinavyotolewa mwishoni mwa maelekezo, ni mapendekezo ili kuwezesha zoezi liwe vizuri iwezekanavyo, lakini jisikie huru kulifanya kwa njia tofauti unazodhani zitakufaa au vizuri zaidi kwa kundi lako.

Bila shaka, unaweza kuongeza mazoezi yako mwenyewe kwenye programu hii. Kwa njia hii, sanduku la zana litakua na kwa kubadilishana mazoezi na wengine, mwongozo wa kazi utatolewa kwa njia nzuri zaidi kwa vijana wa Zanzibar na Tanzania.

**Muundo sawa katika mazoezi yote**
Mazoezi yote yanaelezwa kwa kina zaidi, kufuata muundo huo huo. Hii itakusaidia kuandaa na kuwezesha mazoezi uliyoyachagua. Muundo ni:

**Lengo:** Ni lipi madhumuni ya zoezi? Matokeo gani yatakuwa yanatarajiwa. Kuangalia ufahamu, tabia, ujuzi na vitendo?

**Maandalizi:** Kama mwalimu/mkufunzi, nini cha kufanya katika maendeleo ya kazi kwa ajili ya kutoa zoezi kwa namna ya kuzingatia mchakato? Jinsi ya kuandaa darasa kuwapa washiriki wako eneo wanalohitaji ili kufanya mazoezi? Baadhi ya mazoezi yanahitaji eneo zaidi au mpangilio tofauti wa viti/meza.

**Maelezo:** Kama mwalimu/mkufunzi, nini unaweza kuwaambia wanafunzi/watafutaji wa kazi wako na wabunifu wa kazi kama ni utangulizi kwenye zoezi?

**Utendaji:** Ni nini wanafunzi/watafutaji wa kazi na watoaji wa kazi watalazimika kufanya au kuonesha katika zoezi hilo? Hapa, unaweza kupata mlolongo wa hatua ambazo washiriki huchukua ili kukamilisha zoezi.

**Tafakuri:** Mwaswali gani unauliza mwishoni mwa zoezi (au baada ya hatua mahsusi wakati wa zoezi)?

**Dondoo:** Vitu ambavyo unahitaji kuwa na uelewa navyo wakati wa zoezi.

**Uchunguzi wa kina:** Nini kinaweza kufanywa zaidi kulipa zoezi (kwenda) kina zaidi au kuliunganisha na zoezi jengine?

**Karatasi za mazoezi:** Misaada ya kujifunza, malighafi na vifaa ambavyo vinaweza kutumika na wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi.

# MADA YA 2

# MAELEZO YA JUMLA YA MAZOEZI 'GUNDUA SHAUKU YAKO'

**Gundua shauku yako**
Katika mada ya 2 utakuta mazoezi 14 kuhusu umahiri wa kazi 'Gundua shauku yako': tafakari kuhusu hamasa.

Gundua shauku yako inamaanisha: kufikiria kuhusu matarajio yako na maadili ambayo ni muhimu kwa kazi yako. Wanafunzi/watafutaji wa kazi na wabunifu wa kazi wanakuwa na uelewa ya kile wanachodhani ni muhimu katika maisha yao, elimu na kazi yao. Watagundua kinachowapa hisia za kuridhika, wanachopenda au wasichopenda na kile ambacho (bado) wanahitaji kuendeleza kulingana na matarajio yao.

Katika maelezo ya jumla ya mada ya 2 unaweza kujua wakati na shughuli unapojisikia vyema sana; kutumia ubunifu wako kujielezea juu ya hamu na shauku; kugundua maadili makuu ya kazi na kazi yako bora; kuhadithia hadithi yako na kufanya mipango kwa ajili ya maisha, kipi ni muhimu kwao?

Nambari ambayo zoezi hilo linaendana na idadi ya maelezo ya kina ya zoezi hilo na ya karatasi za zoezi. Karatasi za zoezi zinaweza kunakiliwa kwa urahisi kwa ajili ya vijana wako. Hakikisha unatoa daftari ambapo washiriki wanaweza kuandika matokeo yao na wanaweza kuhifadhi matokea na maendeleo yao. Kwenye gamba la daftari, unaweza kuweka dira ya kazi au washiriki wanaweza kubuni ukurasa wao wenyewe wa mbele.

| Mazoezi 'Gundua shauku yako' | Lengo la zoezi | Mbinu shirikishi |
|---|---|---|
| 2.1 **Nyakati nyekundu na nyakati za kijani** | Vijana wanapata ufahamu juu ya mambo yanayopandisha au kushusha nguvu katika kazi zao za kila siku. | Kutunza kitabu cha kumbukumbu ndani ya wiki kuelezea nyakati nyekundu na nyakati za kijani kila siku. Vijana watajadili na kutoa taswira juu ya nyakati hizi na shauku zao katika vikundi vya watu wawili wawili na katika kundi zima. |
| 2.2 **Nini unachojivunia? Nini unachokijutia?** | Vijana wajifunze uhusiano uliopo kati ya uwezo wao na utendaji wao, ule wanaojivunia na ule wanaoujutia. | Maswali makuu mawili ya kutoa taswira au kujibiwa na vijana. Majibu yatajadiliwa katika kikundi kidogo au baina ya kila kijana na mkufunzi. |
| 2.3 **Kutafuta hazina ya nyakati za dhahabu** | Vijana wanakumbuke nyakati za dhahabu katika maisha yao: nyakati ambazo wanatambua shauku zao. | Vijana watachimba ndani ya kumbukumbu zao kupitia maswali yaliyo katika kadi, kutafuta hazina (nyakati za dhahabu). Wanajifunza nini kutokana na nyakati hizo ukilinganisha na shauku zao na hamasa yao? |
| 2.4 **Chora katuni ya shauku yako!** | Vijana waelezee shauku zao na matarajio yao kwa ufupi katika njia ya uchoraji wa katuni. | Vijana, kila mmoja akiwa peke yake, wachore katuni zao katika taswira tano tu ambapo ndani yake wanajibu swali. Mfano 'nini kinachokufurahisha kuamka kitandani kila siku?' |
| 2.5 **Nguvu ya mandala** | Vijana watengeneze 'nia mandala' ambapo wataona shauku yao kwa ajili ya jambo jipya; wanaonyesha hali yao ya sasa na vipaji vyao na nini wanachohitaji kiendelezwe ili kutimiza malengo yao. | Vijana waeleze sehemu nne za malengo yao (matakwa yao, mahitaji yao, walichonacho kwa sasa na sababu ambayo imeyafanya malengo yao kuwa hayajatimia hadi sasa), kwa kutumia rangi michoro au maneno. |
| 2.6 **Barakoa yangu: sehemu ya ndani na sehemu ya nje** | Vijana wagundue uhusiano kati ya sehemu ya ndani na sehemu ya nje. | Kwa kuleta barakoa au karatasi iliyochapishwa na kupambwa kwa rangi pande zote, vifaa vya asili au maneno, vijana waoneshe sehemu ya ndani na pia sehemu ya nje. |

| | | |
|---|---|---|
| **2.7**<br>**Kauli mbiu yangu katika maisha!** | Vijana wachunguze shauku zao (moyo) na uzoefu wao, kuwa shauku pia huhitaji kufikiria (kichwa), ili kuweza kutoa dira ya kudhihirisha shauku zao. | Kwa kujadili kwa kina katika makundi ya watu wawili wawili kuhusu shauku, kwa kujibu maswali mmoja mmoja na kwa kujaza katika jedwali la mpango kuhusu mawazo/moyo/shauku na kufanya/kichwa/kufikiri/kutoa taswira, vijana wapate muafaka wa kauli mbiu, kauli binafsi. |
| **2.8**<br>**Ndoto** | Vijana wajue uhusiano kati ya vipaji na ndoto zao na wajue jinsi ya kuelezea matarajio yao, matumaini na ndoto zao kuhusu maisha yao ya baadaye. | Maono: Fikiria kuwa ni ya miaka 5 au kumi baadaye, ndoto zako zote zimekuwa kweli. Unaona nini? Baada ya maono hayo vijana washirikishe wenzao uzoefu wao na kutoa hitimisho juu ya kile walichokigundua kuhusu shauku zao. |
| **2.9**<br>**Maadili makuu ya kazi yangu** | Vijana wafikiri na kuwasiliana kwa maneno yao wenyewe juu ya maadili waliyonayo akilini mwao wanapowaza kuwa na utaalamu, kazi au biashara yao. | Tengeneza seti za kadi za maadili na vijana wachague kadi nane ambazo zinawakilisha maadili yao ya kazi. Kisha waziwekee vipaombele kadi hizo na kuelezea katika makundi madogo kuhusu mpangilio wake na kwanini maadili hayo ni muhimu kwao. |
| **2.10**<br>**Ipi kazi iliyo bora kwangu?** | Vijana waandike kazi wanazozitamani katika karatasi au kidigitali. | Kufikiri kwa upana kuhusu kazi iliyobora (mada kama: wapi, katika hali ipi, pamoja na nani, vifaa vipi, mshahara n.k.). Watengeneze bango au watumie programu ya komputa ya pawapointi kuielezea kazi yao iliyo bora. Wachukue picha ya bango kwa kutumia simu zao za mikononi. |
| **2.11**<br>**Dhima yangu katika maisha sehemu ya 1: kugundua shauku na dhima katika maisha** | Vijana wachunguze shauku na dhima zao katika maisha. | Zoezi la maono yaliyowezeshwa. Wakikaa katika duara huku wakiwa wamefumba macho (au wakiangalia mahali fulani au ukutani au sakafuni); vijana wasikilize maandishi ambayo wamealikwa kuingia ndani ya nyumba. Kuna milango mitatu na kila mlango unaelelekea chumbani. Katika kila chumba kuna mtu ambaye vijana wanaweza kumwuliza maswali kuhusu dhima yao. Baada ya maono hayo vijana wachore kile walichokiona. |
| **2.12**<br>**Dhima yangu katika maisha sehemu ya 2: anzisha dhima yako** | Vijana waanzishe dhima zao katika maisha. | Kwa msaada wa maswali na majadiliano ya kina, kuzungumza kuhusu mambo muhimu zaidi katika maisha, kila mshiriki anaandika dhima ya maisha. Vijana wabadilishane na kujadili dhima zao katika kundi. |
| **2.13**<br>**Nguvu ya kufanya kazi** | Vijana wapitie uzoefu kuwa katika kazi na majukumu mbalimbali kuna vitu ambavyo huathiri kiwango cha nguvu ya utendaji kazi na shauku. | Wakiwa mmoja mmoja waorodheshe orodha ya shughuli zao za kila siku kwa siku ya kazi kwa taaluma wanayoisomea. Kisha waorodheshe mambo ambayo huwafanya wawe na furaha na yale ambayo huwafanya waishiwe nguvu. Vijana wajadili matokeo yao katika makundi ya watu wawili wawili. |
| **2.14**<br>**Nguvu ya kufanya kazi** | Mwishoni mwa mafunzo vijana watengeneze habari kuhusu matukio muhimu katika miaka (mwaka) ambapo walipata au walikutana na shauku zao. | Baada ya maandalizi yanayosaidiwa na maswali kadhaa, waelezee habari yao kwa dakika 3 (watengeneze video kutokana na habari hiyo kwa kutumia simu za mkononi kama wanazo).. |

2.1

# NYAKATI NYEKUNDU NA NYAKATI ZA KIJANI

**Lengo**
Vijana wanapata ufahamu juu ya mambo yanayopandisha au kushusha nguvu katika kazi zao za kila siku.

**Maandalizi**
Agiza vijana kuleta daftari ambalo linawavutia au waagize waanze kuandika jarida kwa kutumia simu zao (mfano kwa kutumia programu tumishi ya evanote).

**Maelezo**
'Kugundua sababu ya kiwango cha nguvu kushuka au kupanda katika masomo unayofuatilia na katika maisha ya kila siku. Utaanza kuandika jarida kwa wiki moja. Utaandika nyakati zinazokupotezea nguvu na nyakati zinazokuongezea nguvu. Unahitaji kutumia dakika tano tu za muda wako kufanya jambo hilo kila siku. Wiki ijayo tutajadili kile ulichokiandika. Kutunza jarida katika mtindo huu kutasaidia kujua shauku (na kipaji chako) zako zilipo.'

**Utendaji**

1. Agiza vijana kutunza jarida katika daftari au katika simu ya mkononi (mfano kwa kutumia programu tumishi ya evanote) ambamo hutumia kila siku kuelezea nyakati za kijani na nyakati nyekundu. Nyakati za kijani ni nyakati unazofurahia, unasahau habari za muda na hulazimiki kufikiri juu ya kile unachokifanya. Unazitazamia nyakati hizi, hudhani kuwa kile unachokifanya ni cha pekee, lakini watu wengine wanasema kuwa unafanya vizuri kitu hicho. Nyakati nyekundu ni nyakati ambazo zinaonekana kama zinadumu kwa muda mrefu zaidi, hutamani kuzifikia nyakati hizo, zinakuchukulia muda na nguvu nyingi na zinachosha.
2. Agiza vijana kutumia walau dakika tano kwa ajili ya kutunza jarida kila siku.
3. Wape vijana nafasi ya kujipiga picha nyakati za kijani na nyakati nyekundu.

**Ufuatiliaji katika mkutano wa wiki itakayofuata**

4. Tengeneza makundi ya watu 2, 3 au 4.
5. Waruhusu vijana wabadilishane daftari zao na washirikishane:
   - Zipi ni nyakati za kijani kwako, zipi ni nyakati nyekundu?
   - Picha yako uliyojipiga inaonekanaje?
   - Je umeona baadhi ya vitu, je kuna kitu kilichovuta shauku zako?
   - Je umebadilisha kitu fulani katika mwenendo wako kwa sabau ya zoezi hili?
6. Kufuatia mjadala wa nyakati nyekundu na nyakati za kijani, agiza kila kijana kuandika hitimisho mwishoni mwa jarida.

**Tafakuri**
Shirikisha kundi zima jinsi ilivyofanana kuweka taswira ya nyakati za kijani na nyakati nyekundu. Ni nani anapenda kuwashirikisha wenzake hitimisho lake? Je kuna tofauti au mfanano na yale waliyoyasikia kutoka kwa wanadarasa wenzao? Baada ya taswira hiyo, wape vijana nafasi ya kurekebisha hitimisho zao wenyewe. Mwishoni unaweza kufunga zoezi kwa kuuliza zipi ilikuwa nyakati nyekundu na nyakati za kijani kwa kila mwanafunzi katika somo hili.

***Dondoo***

Tengeneza kundi katika moja kati ya mitandao ya kijamii ambapo utakuwa unatuma ujumbe kila siku ukiuliza: umefanya tathmini ya nguvu zao leo? Tunza jarida la nyakati nyekundu na nyakati za kijani wewe mwenyewe. Utalitumia siku za baadaye, utakapokuwa ukiwaeleza wenzio katika kundi jinsi ulivyotumia nguvu zako kwa wiki nzima.

# 2.2

# NINI UNACHOJIVUNIA? NINI UNACHOKIJUTIA?

**Lengo**
Vijana wajifunze uhusiano uliopo kati ya uwezo wao na utendaji wao, ule wanaojivunia na ule wanaoujutia.

**Maandalizi**
Panga viti na meza kwa namna ambayo vijana wanaweza kufanya kazi mmoja mmoja au katika makundi ya wawili wawili au wanne wanne.

**Maelezo**
'Zoezi hili linahusu vitu unavyovijutia na vitu unavyojivunia. Utatoa taswira ya uzoefu wako. Unaweza kujifunza kutoka humo, hasa pale unapoyavutia taswira kutoka mbali. Itakuwa ni kuhusu mambo chanya na mambo hasi ambayo ulihusika nayo moja kwa moja. Kuhusu kitu ulichokifanya, na siyo kile unachokifanya sasa. Mafanikio yako yanasema kitu fulani kuhusu ujuzi wako, sifa zako na shauku zako.'

**Utendaji**
1. Agiza vijana, kila mmoja kwa ajili ya wengine, kufikiri juu ya hali fulani na kuelezea kitu wanachojivunia. Waulize kujibu maswali yafuatayo:
   - Ulifanya kitu gani hasa katika hali ile?
   - Hiyo inakuambia nini kuhusu sifa zako, ujuzi wako na shauku zako?
   - Ulifanya nini hasa, kinachokufanya useme: 'Sawa, hiki ndicho kitu ninachojivunia?'
2. Uliza vijana juu ya hali fulani na kuelezea jambo fulani ambalo wanalijutia. Watake vijana kujibu maswali yafuatayo:
   - Nini kilitokea?
   - Ulifanya nini?
   - Kitu gani katika hali hii kinakufanya uijutie?
   - Ni kitu gani ambacho ungelipenda kukifanya tofauti?
   - Katika sifa zako, ni zipi ambazo zingefaa zaidi kuzitumia katika hali hii?
3. Waruhusu vijana kushirikishana hali zao na majibu yao katika makundi ya wawili wawili. Ruhusu washirikishane walichojifunza kutoka katika taswira hizi na katika kushirikishana huku. Agiza vijana kufikiri juu ya hali fulani wiki ijayo ambayo wataonesha sifa zao njema na uwaambie waandike matarajio yao.

**Tafakuri**
Uliza vijana wanajisikiaje wanapopata taswira kwa namna hii katika hali fulani? Nini kinawasaidia kushughulika na hali hiyo wakati mwingine? Je, kuna vitu ambavyo wanaweza kuvifanyia mazoezi kesho au wiki ijayo? Kama ndivyo, weka ahadi na vijana hao kuweka katika ratiba yao ya masomo katika kipindi kijacho au kuwa na majadiliano ya mwanafunzi mmoja mmoja na mwalimu.

***Dondoo***

Katika zoezi hili, ni muhimu vijana kuelewa kuwa hali wanazopitia zinaweza kuwekwa katika mchakato wa kujifunza. Hili zoezi halihusu kuamua mambo kwa haraka. Linawafanya vijana kwa upana kujua hali wanazopitia zaweza kuwekwa katika majadiliano, ili waweze kupata uzoefu kuwa taswira ya majadiliano inaweza kupelekea kwenye majibu au uamuzi. Na wanapojutia jambo, taswira inawaambia kuwa sifa nyingine zinaweza kutumika kwa manufaa zaidi katika hali inayofanana siku za baadaye.

# 2.3

# KUTAFUTA HAZINA YA NYAKATI ZA DHAHABU

KARATASI YA ZOEZI 2.3

**Lengo**
Vijana wanakumbuka nyakati za dhahabu katika maisha yao: nyakati ambazo wanatambua shauku zao.

**Maandalizi**
Panga meza na viti kwa namna ambayo vijana watafanya kazi katika makundi ya watu wanne. Hakikisha una karatasi za kutosha ya zoezi 2.3 'Kutafuta hazina ya nyakati za dhahabu'. Unahitaji kuandaa karatasi za zoezi na kuziweka ndani ya bahasha kabla ya zoezi. Unapohitaji seti mpya ya kadi, unaweza kuipakua kutoka www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet. Utakuta viunganishi kwenye programu ya Maendeleo ya Kazi, Mada hii na karatasi hii ya zoezi.

**Maelezo**
'Nyakati katika maisha ya zamani ambazo zilikuamsha, zilikuongoza katika kuelekea katika shauku zako, nyakati za bubujiko lako na zilizokufanya uwe na furaha. Nyakati ambazo zina thamani kubwa zaidi, ambazo ulipata uzoefu wake kupitia viungo vyote vya ufahamu: kusikia, kuona, kunusa, kuonja na kugusa. Elezea nyakati hizo kwa namna ambayo ni kama vile zimetokea sasa hivi. Mfano: natembea katika msitu na napata harufu ya vitu asilia. Naona kipepeo akitua katika maua.'

**Utendaji**
1. Wapange vijana mezani katika makundi ya watu wanne na uwagawie karatasi ya zoezi 2.3 'Kutafuta hazina ya nyakati za dhahabu'.
2. Kila kundi lina seti ya kadi, zilizo na neno 'shauku' juu yake na maswali yakigeuziwa upande wa meza.
3. Kijana anageuza kadi na kusoma swali. Uliza kama hii inavuta kumbukumbu ya mbali. Kijana atasoma swali kwa sauti na kuchagua kulijibu mwenyewe au kuchagua mtu mwingine kulijibu. Muda wote kijana anaweza kufaulu.
4. Kijana aandike majibu yanayotoka akilini mwake kwa maneno machache.
5. Vijana warudie zoezi hili mara kadhaa.
6. Baada ya marudio hayo, waangalie kile walichokiandika. Vijana wapigie mistari maneno muhimu, maneno yanayojirudia mara kwa mara, maneno ambayo yana maana maalumu kwao au yenye msisitizo mkubwa.

**Tafakuri**
Uliza vijana jinsi walivyojisikia kuhusu zoezi hili na nini ambacho limewafundisha. Wanaweza kuandika maneno muhimu katika karatasi kuukuu. Au wanaweza kutumia kifaa cha kidigitali (www.answergarden.ch): ambapo maneno yanayotumika sana yataonekana katika skrini. Je maneno haya yanahusishaje shauku za vijana na kazi zao?

***Dondoo***
Husika katika zoezi hili au liandae ukiwa nyumbani. Waweza kuwa mfano au kwa kuwaonesha vijana ni kwa namna gani unaitii haja ya moyo wako. Endapo itahitajika, tengeneza kadi kwa ajili yako mwenyewe ambazo unaona zitafaa zaidi kwa ajili ya kundi lako.

# 2.4 CHORA KATUNI YA SHAUKU YAKO

**Lengo**
Chora katuni ya shauku yako

**Maandalizi**
Hakikisha vijana wana penseli, gum au peni. Unapaswa kujua mapema ni swali linapaswa kujibiwa na ni kwa makusudi yapi. Unapaswa kutoa maswali uliyoyapendekeza kwa wanafunzi, ambamo toka kwayo watachagua maswali ya kujibu. Baadhi ya maswali yaweza kuwa:

- Nini kinakufurahisha kuamka kitandani kila siku?
- Ni kwa matatizo yapi wewe ni jawabu?
- Unajivunia nini?
- Watu wangeweza kijifunza nini kutoka kwako?
- Ungetamani watu wengine wakuchukulieje?
- Kuna nini katika orodha ya matarajio yako?
- Unatamani kufanya kazi na nani siku moja?

**Maelezo**
'Katika zoezi hili tutatafsiri vipaji vyetu na matarajio yetu kuwa mchoro wa katuni. Hatutajibu swali kwa maneno, lakini kwa namna ya katuni. Jibu la swali linatakiwa kueleweka mapema, yasihitajike maelezo mengine.'

**Utendaji**
1 Waruhusu vijana kuchagua swali moja wapo kati ya maswali ya hapo juu au mwalimu awachagulie.
2 Vijana wajibu swali kwa mtindo wa mchoro wa katuni. Mwongozo ni kuwa, jibu la swali liwe lenye kueleweka mapema, yasihitajike maelekezo mengine. Unaweza kutumia michoro mitano tu, si zaidi ya hapo.
3 Agiza vijana wanapomaliza michoro yao kuwaonesha wenzao darasani, waagize wapeane mrejesho kila mmoja kwa mwenzake ili waweze kuboresha michoro yao ya katuni.

**Tafakuri**
Vijana wazielezee kanda zao za katuni. Uliza maswali kuhusu kile unachokiona katika ukanda wa katuni. Walilenga kuonesha nini? Walipata mrejesho gani kutoka kwa wanafunzi wenzao? Uliza kama washiriki wengine wanaweza kuongeza kitu katika maoni hayo. Hakikisha hutoi hukumu juu ya katuni lakini uliza maswali.

***Dondoo***
Hili haliwezi kuwa zoezi jepesi kwa vijana, hasa hasa kama hawana uzoefu wa kuzisoma au kuzielewa katuni. Lete baadhi ya katuni toka Tanzania au Zanzibar. Wafanye wanafunzi wajue kuwa siyo lazima michoro ya katuni kuwa mizuri. Kinachohitajika ni wao kuwa na uwezo wa kujiangalia kwa namna tofauti. Yawezekana pia vijana wakatengeneza katuni za kidigitali kwa kutumia simu, kompyuta mpakato au komputa ya mezani.

# NGUVU YA MANDALA

KARATASI YA ZOEZI 2.5

**Lengo**
Vijana watengeneze 'nia mandala' ambapo wataona shauku yao kwa ajili ya jambo jipya; wanaonesha hali yao ya sasa na vipaji vyao na nini wanachohitaji kiendelezwe ili kutimiza malengo yao.


**Maandalizi**
Pangilia chumba utakachotumia kwa namna ambayo vijana wataweza kufanya kazi kwa kutumia karatasi kubwa (A3). Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 2.5 'Mandala yangu'. Kusanya vitendea kazi vya kutosha: karatasi, penseli au chaki za rangi na vitu vya duara kwa ajili ya kuchorea miduara.


**Maelezo**
'Inaonekana kama anasa ya kisasa: kuvuta taswira ya mambo fulani ambayo unahitaji kufanikiwa maishani na ambayo ni ya maana kwako. Lakini ubinadamu, katika tamaduni zote, ni kuyafanyia kazi maudhui haya kwa karne nyingi. Muundo unaojirudia mara kwa mara ambao watu huonesha ndoto zao na haja zao kuwa, huitwa mandala. Mandala ni miduara ya kimazingaombwe ambayo huchorwa au kurembeshwa kwa namna maalum. Mandala yanaweza kupatikana miongoni mwa kabila la Waaboriginal huko Australia ambao walichora ndoto zao katika mchanga, na pia kwenye madirisha ya mviringo ya makanisa ya Kikristo na makanisa ya Kiaskofu. Mandala huchorwa kwa miduara, kuwakilisha thamani ya 'nafasi ya ndani' (mambo ya ndani yanayowezekana). Kushughulikia eneo hili muhimu husaidia kupata umaizi na amani. Leo tunatengeneza mandala yetu wenyewe.'

**Utendaji**
1 Kijana achore duara kwenye kipande kikubwa cha karatasi (A3) na kuligawa duara hilo katika sehemu nne. Kama inavyoelezwa katika karatasi ya zoezi 2.5 'Mandala yangu'.
2 Waagize kuchora 'nia mandala' sehemu moja ya mpango wa baadaye (nia), sehemu nyingine kinachohitajika ili kutimiza mipango hiyo ya baadaye, sehemu nyingine vitu ambavyo vipo tayari kwa ajili ya kutimiza mipango hiyo ya baadaye na sehemu nyingine vitu ambavyo vinahafifisha nia au mipango hiyo ya baadaye.
3 Vijana wakiwa tayari, wape nafasi ya kueleza mandala yao katika makundi ya watu wanne.

**Tafakuri**
Jadili mandala katika makundi ya watu wanne. Unaonaje namna hii ya kuelezea shauku zao? Waruhusu kushirikishana kile walichokiweka kwenye karatasi na vile kinavyomaanisha kwao. Umegundua jambo fulani katika zoezi hili? Katika kundi zima, mnaweza kushirikishana uzoefu mlioupata kwa kuchora mandala.

***Dondoo***
Andaa zoezi hili kwa kulifanya mwenyewe nyumbani, ili uwaoneshe vijana mandala yako. Tengeneza mandala nyingine ukiwa darasani, ili kuonesha kuwa mandala hutofautiana siku hadi siku, nyakati na nyakati. Weka muziki wa taratibu kwa mbali. Agiza vijana kutohukumu kile wanachokichora au kukipaka rangi, kila kitu ni kizuri! Ni kuhusu kuelezea mawazo na shauku na siyo kwa ajili ya kuwahukumu.





Artwork Vecteezy.com

# 2.6

# BARAKOA YANGU: SEHEMU YA NDANI NA SEHEMU YA NJE

KARATASI YA ZOEZI 2.6

**Lengo**
Vijana wagundue uhusiano kati ya sehemu ya ndani na sehemu ya nje.

**Maandalizi**
Panga darasa lako kwa namna ambayo vijana wanakuwa na eneo pana la kufanyia kazi: kukata, kuchora na kupaka rangi. Fanya kuwa jukumu la pamoja, kukusanya vifaa vingi iwezekanavyo kuipamba barakoa na michoro iliyochorwa. Katika majarida unaweza kutafuta maneno, picha na michoro. Mazingira asili yanakupa vitu vingi ambavyo unaweza kutumia. Unaweza kutumia majani, matawi ya miti, manyoya, mbegu n.k. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 2.6 'Barakoa yangu: sehemu ya ndani na sehemu ya nje' au andika maelezo katika ubao.

**Maelezo**
'Kama wanadamu huwa hatuwezi kuonesha uhalisia wa nafsi zetu. Wote tuna majukumu anuai, kama binti/kijana, dada/kaka, rafiki, mwanafunzi/mwajiriwa. Mienendo yetu hutegemea majukumu tunayoyatekeleza. Mienendo yetu hutofautiana pale tunapokuwa na rafiki na pale tunapokuwa kazini. Si hivyo tu, hatumwoneshi kila mtu jinsi tulivyo kiuhalisia. Wakati mwingine hatupendi tu kuwaonesha, lakini pia kwa sababu mara nyingi haipendezi. Katika zoezi hili utafanya kazi na pande mbili za kwako wewe mwenyewe. Ni mambo gani ambayo unapenda kuwaonesha wengine na ni yapi ambayo unapenda kubaki nayo mwenyewe? Hutoyaeleza haya kwa njia ya maandishi, bali utatengeneza barakoa au mchoro wa kwako mwenyewe.'

**Utendaji**
1. Waruhusu vijana watengeneze barakoa ya uso wao wenyewe au wachore picha ya mikono yao wenyewe.
2. Kisha, waagize kufanya sehemu ya ndani na sehemu ya nje ya barakoa au mchoro, wakifuata maelekezo yaliyoko katika karatasi ya zoezi 2.6 'Barakoa yangu: sehemu ya ndani na sehemu ya nje'.
3. Waruhusu waandike maneno ambayo wanadhani yanaoana na sehemu ya ndani na yale yanayooana na sehemu ya nje. Waruhusu kutumia vitu walivyokusanya kutoka kwenye majarida au mazingira asilia kuelezea pande hizo mbili.
4. Waagize kuandika majina yao katika sehemu ya nyuma ya upande wa ndani na ya upande wa nje.
5. Vijana wachukue picha za barakoa zao au michoro yao na waandae maonesho.

**Tafakuri**
Tembelea eneo la maonesho pamoja na vijana wakuelezee kazi zao. Kwanini walichagua namna hii? Wamepitia uzoefu gani katika zoezi hili? Walijisikiaje kuelezea undani wao na upande wa nje wao kwa kutumia ubunifu wa sanaa? Je, wameona jambo lolote jipya kuwahusu wao wenyewe katika zoezi hili?

***Dondoo***
Andaa maonesho ili kuonesha matokeo ya zoezi hili ili kila mmoja aweze kuona barakoa na michoro ya mwenzake.

**Uchunguzi wa kina**
Agiza vijana kuandika habari yenye kichwa: 'nikivua barakoa yangu...' au 'ukiangalia sehemu ya ndani ya mkono wangu...' wanaweza kutumia taswira ya zoezi hili kuandika habari yao.

# KAULI MBIU YANGU KATIKA MAISHA!

KARATASI YA ZOEZI 2.7

**Lengo**
Vijana wachunguze shauku zao (moyo) na uzoefu wao kuwa shauku pia huhitaji kufikiria (kichwa), ili kuweza kutoa dira ya kudhihirisha shauku zao.

**Maandalizi**
Andaa zoezi hili kwa kulifanya mwenyewe, ili uweze kujiandaa kwa maswali ambayo vijana wanaweza kukuuliza. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 2.7 'Kauli mbiu yangu katika maisha' na karatasi nzuri za A4 zenye rangi.

**Maelezo**
'Shauku ni muhimu sana kwa binadamu: zinakuonesha vile ulivyo. Shauku ziko ndani ya kila mtu, zipo kila wakati. Wakati mwingine hazikupata nafasi ya kujionesha zikabaki nyuma ya pazia. Shauku zinaweza kuvumisha maisha mapya kuwa haja na nguvu zilizosahaulika muda mrefu. Watu wengine hawapendi neno 'shauku', wanapenda kutumia maneno kama 'msukumo', 'nguvu' au kitu kinachokufanya uwe na 'furaha'. Kuwa na kipaji katika jambo fulani haimaanishi kuwa kila wakati unapenda kulifanya jambo hilo. Chukua vipaji vyako vikubwa - ambavyo ungependa kuvitumia kama - vianzio katika maendeleo yako binafsi. Utaendelea kwa kasi na huku ukiwa na furaha zaidi.'

**Utendaji**
1 Vijana wajadiliane wawili wawili kuhusu neno 'shauku'. Lina maana gani kwako? Linakufaa?
2 Uliza vijana, ni neno lipi linawafaa zaidi: 'shauku', kitu kinachonifanya kuwa na' furaha', kitu kinachonipa 'msukumo', 'nguvu' au neno jingine tofauti.
3 Wapatie mpango kwenye karatasi ya zoezi 2.7 'Kauli mbiu yangu katika maisha'. Washiriki watakiwe kujaza maswali yafuatayo.
   - Ni lini ulipitia uzoefu wa shauku? Ni lini moyo wako na kichwa chako kiukweli vilikubaliana? Andika kazi hii katika mraba wa juu kushoto. Itakuwa ni kazi ambayo kiukweli imeunganishwa na jinsi wewe ulivyo na kuwa bila wasiwasi unaijua vizuri.
   - Ni lini ulifanya kitu kwa kutumia kichwa chako, bila uhiari wa moyo wako? Ni wakati gani ulifanya kitu fulani kwa sababu tu umetakiwa kufanya? Andika hii katika mraba wa upande wa juu kulia.
   - Ni lini ulifanya kitu unachokijutia, kitu ambacho ulijua si chema kwako na wala hakikukufanya kuwa na furaha? Andika hili katika mraba wa chini kulia.
   - Lini ulifanya kitu kwa moyo wako? Kitu ambacho kiukweli hukukifikiria, ukakifanya kwa msukumo, bila kujali madhara (chanya au hasi) ambayo yangeweza kujitokeza. Andika hii katika mraba wa chini kushoto.
4 Agiza kila kijana kujadili mpango wake na mwenzake. Baada ya hapo vijana waweze kujibu maswali yafuatayo katika kipande cha karatasi.
   - Mpango wako uliokamilishwa unakuambia nini?
   - Haja yako ni ipi?
   - Nini ambacho kingekusaidia kesho?
   - Unahitaji kuwa na nini? Kuna mahitaji gani yanapaswa kuachwa au kuna mahitaji gani yanapaswa kuongezwa?
   - Nia yako yaweza ndoto yako muhimu ya kufanya kitu kizuri. Inaweza kuwa pia nia ya kuwa na maisha yakujitosheleza ya kila siku, ambayo inaanza sasa.
   - Nia yako yaweza kuwa swali lakufanyiwa utafiti: nataka kufanya utafiti ... namna ganii/ nini/kwanini/...'
5 Waruhusu vijana wapitie tena majibu yao na uwatie moyo ili waweze kuibuka na kauli mbiu.
6 Kauli mbiu (katika maisha) ni ujumbe mfupi, tamaa, nukuu inayoeleza ni nini mtu anathamini katika maisha.
7 Vijana waandike kauli mbiu kwa herufi nzuri kwenye karatasi za rangi za A4 katika muundo wa kigae. Weka kauli mbiu ukutani na kila kijana aweze kuelezea kauli mbiu yake.

**Tafakuri**
Elekeza vijana kuelezea kauli mbiu zao. Uliza jinsi wanavyofikiria juu ya kuziangalia shauku zao kwa namna hii, ambapo wanaona kuna uhusiano kati ya moyo na kichwa.

***Dondoo***
Tambua kuwa vijana wanaweza kutumika kujiangalia wenyewe katika namna hii. Wape nafasi ya kulifanyia mazoezi zoezi hili. Na hakikisha unaweka bayana kuwa zoezi hili halilengi kutatua matatizo, bali ni sehemu ya mchakato ambao vijana wanapitia katika ukuaji wao. Fikiria kauli mbiu yako mwenyewe, ili uweze kuwa mfano kwa vijana. Wasisitizie vijana kuwa shauku siyo kitu ambacho unakifanya moyoni tu. Kiukweli, unapoishi kutoka moyoni tu, kiukweli unapokuwa na shauku za moyoni tu. Kutia mkazo kwa ajili ya vijana kwamba shauku sio kitu unachokifanya kwa moyo wako pekee, unajiweka kwenye uwezekano wa kuingia katika mazingira ya hatari na yasiyofaa. Kwa mfano, unapozama baharini katika eneo ambalo maji ni mafupi, au unajiingiza kwenye masuala ya mapenzi bila ya kuwa mwangalifu, au unapokaa na kuongea na marafiki usiku kucha ili kupoteza muda ambao ungeutumia kwa ajili ya kazi za nyumbani. Majuto yaweza kuwa ni kielelezo kuwa ulifuata moyo tu (na siyo kichwa).

# 2.8 NDOTO

**Lengo**
Vijana wajue uhusiano kati ya vipaji na ndoto zao na wajue jinsi ya kuelezea matarajio yao, matumaini na ndoto zao kuhusu maisha yao ya baadaye.

**Maandalizi**
Weka viti katika mduara, bila meza, ili vijana waweze kuonana toka kichwa hadi kidole cha mguuni.

**Maelezo**
'Unapokuwa na wazo zuri la sifa zako, ni vyema kuwa na ndoto ya namna utakavyolitekeleza wazo hilo. Hili ndilo ambalo tutaliangalia katika zoezi hili.'

**Utendaji**
1. Agiza vijana kukaa katika viti ambavyo umevipanga kwenye mduara. Waambie wajishushe huku miguu yao yote ikiwa aridhini.
2. Waambie vijana kuwaza ndoto ya namna na kutumia sifa zao kwa kiwango cha hali ya juu iwezekanavyo. Waagize wafumbe macho na kulenga mahali fulani ndani ya chumba. Mwanzoni wanahitaji kuvuta na kutoa hewa nje taratibu na mara chache.
3. Waalike vijana kuangalia ndani yao na uwaulize waziangalie ndoto zilizowajia katika akili zao huku ukiwauliza maswali yafuatayo:
   - Hebu fikiria una miaka mitano au kumi zaidi, ndoto zako zote zimekuwa kweli.
   - Uko wapi? Uko na nani?
   - Nyumba yako inafananaje?
   - Unafanya nini?
   - Nini unachojivunia?
   - Mambo gani umefanikiwa kuyatimiza?
   - Unafanya kazi gani?
   - Nini ndoto zako kwa ajili ya maisha ya baadaye zaidi?
4. Agiza vijana taratibu kurudi kwenye wakati wa sasa. Agiza vijana kutembeza miguu yao na mkono yao na kisha kufumbua macho taratibu, kurudi katika kundi na kuangalia hapa na pale.

**Tafakuri**
Jaribu kutofautisha, na kung'amua vitu muhimu zaidi katika habari ambazo vijana wanazokuambia. Wape mambo hayo muhimu zaidi kama maoni kwa habari wanazokupatia. Nini ambacho unakisoma katika habari zao? Nini ambacho vijana wanagundua bila kujielewa katika kuhusu umuhimu wao? Wape nafasi ya kuandika mafunuo yao muhimu zaidi.

***Dondoo***
Wape vijana nafasi ya kuifikiria ndoto yao mara nyingi iwezekanavyo. Uwaambie kuwa hakuna mipaka. Wape muda wa kuzifikiria ndoto zao katika maswali mengi. Huu ni aina ya muongozo wa maono, pia angalia zoezi la 2.11 kwa ajili vidokezo zaidi.

**Uchunguzi wa kina**
Zoezi hili linaweza kuongezewa kazi nyingine mpya. Uliza vijana kama wanaweza kutengeneza kielelezo cha shauku (mood) cha ndoto zao au watengeneze mkusanyiko wa picha katika simu zao. Unaweza kutumia zoezi hili kama sehemu ya maonesho katika kusherehekea hitimisho la mafunzo yao. Unaweza pia kutumia matokeo ya zoezi hili kama kichocheo cha sherehe katika mahafali yao.

# 2.9

# MAADILI MAKUU YA KAZI YANGU

KARATASI YA ZOEZI 2.9

**Lengo**
Vijana wafikiri na kuwasiliana kwa maneno yao wenyewe juu ya maadili waliyonayo akilini mwao wanapowaza kuwa na utaalamu, kazi au biashara yao.

**Maandalizi**
Pangilia viti vyako kwa namna ambayo washiriki wana nafasi ya kutosha ya kutawanya kadi bila kubughudhiwa na kadi za wengine. Hakikisha una seti za kutosha za karatasi ya zoezi 2.9.1 'Maadili ya kazi'. Unahitaji kuwa na karatasi za zoezi zikiwa zimekatwa na kuhifadhiwa kwenye bahasha kabla ya zoezi. Unapohitaji seti mpya ya kadi, unaweza kuipakua kutoka www.vso.nl/cbet na www.vsointernational.org/cbet. Utakuta viunganishi kwenye programu ya Maendeleo ya Kazi, Mada hii na karatasi hii ya zoezi. Hakikisha pia una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 2.9.2 'Maadili ya kazi yangu'.

**Maelezo**
'Siyo kwamba ni muhimu tu kuwa na kazi, lakini kuwa na kazi yenye thamani kwako, inayoleta maana kwako. Kwa namna hiyo yawezekana ukaifurahia kazi yako zaidi ya vile ambavyo ungekuwa na kazi ambayo umeitafuta 'sawa', lakini haikupi hamasa au nguvu ya kuifanya. Ndiyo maana ni muhimu kujifunza namna ya kutafuta maadili muhimu yanayohusu utaalamu, kazi au biashara.'

**Utendaji**
1. Mpatie kila mmoja bahasha yenye seti ya karatasi ya zoezi 2.9.1 'Maadili ya kazi'.
2. Waagize vijana kuweka kadi mezani mbele yao.
3. Waruhusu kuchagua maadili 8 ambayo ni muhimu kwao linapokuja suala la utaalamu, kazi na biashara.
4. Agiza vijana kupanga kadi zao katika mtiririko kulingana na umuhimu. Kwa kuanza muhimu zaidi, muhimu kidogo na kuendelea.
5. Gawa kundi katika vikundi vya watu watatu watatu na waruhusu wajadili mpangilio wa kadi zao za maadili ya kazi. Kwanini walichagua maadili hayo? Tofauti zao ni zipi? Kufanana kwao ni kupi?
6. Waagize vijana kuandika kwa maneno yao wenyewe, wanachomaanisha kwa kila maadili ya kazi waliyochagua, wanaweza kuandika katika karatasi ya zoezi 2.9.2 Maadili ya kazi yangu' wanaweza kupiga picha za mpangilio wa maadili ya kazi kwa kutumia simu zao za mkononi.
7. Wanafunzi wakusanye kadi zote na zirudishwe katika bahasha na uzikusanye bahasha wewe mwenyewe kwa ajili ya kundi jingine.

**Tafakuri**
Uliza vijana kuwa wanafikiri nini kuhusu zoezi hili. Walijifunza nini? Zoezi hili liliwaambia nini? Walifikiria nini kuhusu mpangilio wa vijana wenzao? Waandike mawazo yao kwenye karatasi yao ya mazoezi.

***Dondoo***
Fanya zoezi hili pamoja na vijana au liandae nyumbani. Kwa namna hii, unakuwa kama mfano na kuwaonesha vijana unayofikiri kuwa ni muhimu katika mazingira yako ya kazi. Hii inawapa nafasi nyingine ya kujifunza kitu kingine.

**Uchunguzi wa kina**
Agiza vijana kutumia mpangilio huo huku wakiandika barua ya hamasa kwenda kwa kampuni wanayoijua au watakayoibuni. Katika barua hiyo, kujieleza wenyewe kwa kampuni hiyo (ya kufikirika) bila kujibu au bila kuona tangazo la nafasi za kazi. Wazo hili ni kusema, natamani kufanya kazi na nyinyi. Barua ianze na sentensi ifuatayo: 'Kwa utawala, kama ningekuja kufanya kazi pamoja nanyi, ningetamani kupitia uzoefu ufuatao katika kazi zangu..... .' Wakati huohuo, vijana waandike katika barua zao ni vitu gani wangetamani kampuni ifanye ili kuweza kuyaishi matarajio nao na maadili yao ya kazi. Kwa kufanya zoezi hili mara kwa mara wakati wa mafunzo, vijana watajifunza kuwa maadili yao ya kazi yangekuwa yamebadilika baada ya kipindi fulani. Wataendelea kujitambua vizuri zaidi kila wakati.

# 2.10

# IPI KAZI ILIYO BORA KWANGU?

KARATASI YA ZOEZI 2.10

**Lengo**
Vijana waandike kazi wanazozitamani katika karatasi au kidigitali.

**Maandalizi**
Hakikisha una nafasi ya kutosha ya kufanyia kazi darasani. Vijana wanatakiwa kuweza kukusanya na uwezekano wa kukusanya na kupangilia picha za aina zote kutoka katika intaneti, magazeti, makaratasi na vifaa vya matangazo ya biashara. Wanaweza kulazimika kuwa na meza kubwa zaidi kwa kuunganisha madawati manne. Hakikisha una vifaa vya kutosha kama; karatasi mgeuzo, mikasi, gundi, gundi mkanda, na compyuta iliyounganishwa na projecta. Unaweza kuhitaji kuandaa zoezi hili kwa kulifanya wewe mwenyewe kwanza, ili uwe mfano kwa vijana na uwe umejiandaa kwa aina ya maswali ambayo vijana wanaweza kukuuliza. Kwa njia hii, wanajifunza kuwa hata wewe hupendi nyanja zote za utaalamu wako au huoni kuwa nyanja zote za utaalamu wako zina umuhimu unaofanana. Hakikisha una nakala za kutosha za karatasi ya zoezi 2.10 'Kazi yangu iliyo bora'.

**Maelezo**
'Kuhakikisha kuwa una uwezo wa kupata taswira ya kile unachokifanya wakati wa mafunzo au baadye katika kazi yako, ni vizuri kufikiria kuwa kazi yako iliyobora itakuwaje. Kazi yako iliyo bora siku zote inaunganishwa na moyo wako, usipousikiliza moyo wako kabisa, unaingia kwenye hatari ya kuugua au kuwa na uchungu. Tunahitaji kuwa na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa hali zetu na kulingalisha na hali bora ili tuweze kujua kama tuko katika mstari sahihi. Hiki ndicho ambacho tutakifanya katika zoezi hili.'

**Utendaji**
1. Vijana waielezee kazi yao iliyobora kulingana na maswali yaliyo katika karatasi ya zoezi 2.10 'Kazi yangu iliyo bora'. Watie moyo kuchukua hali iliyobora zaidi kama sehemu ya kuanzia, bila kuwa wa kawaida. Wanaweza kufanya mabadiliko yoyote baadaye.
2. Agiza vijana kukusanya picha kutoka katika majarida au intaneti ambazo zinaoana na maelekezo ya kazi yao iliyo bora.
3. Vijana watengeneze muunganiko wa pamoja wa picha na vitu vingine walivyokusanya. wanaweza kuweka muunganiko huu katika karatasi mgeuzo au kutengeneza onesho kwa kutumia programu ya compyuta ya pawapointi.
4. Weka miunganiko yote ukutani katika chumba cha sanaa au maonesho au onesho kwa kutumia projecta. Waruhusu vijana kutembea kidogo katika kuta na kuangalia ubunifu wao na kuelezana kila mmoja na mwenzake kile walichokifanya.
5. Vijana wachukue picha za ubunifu wao kwa kutumia simu zao za mkononi na kuweka pawaponti zao katika flashi.

**Tafakuri**
Jadili na vijana ubunifu/michoro/picha mbalimbali na uwaulize tofauti au kufanana wanakokuona. Walijifunza nini kutoka katika zoezi hili? Je walijifunza jambo ambalo hawakulielewa hapo awali? Walipata uzoefu gani katika kuiangalia kazi yao iliyo bora kwa namna hii? Je wana maswali mengine baada ya zoezi hili?

***Dondoo***

Hata hivyo hali bora ni 'ujumbe usiowezekana'. Angalau kwa tulio wengi unawezekana. Watie moyo vijana kuelezea hali yao iliyo bora zaidi. Siyo suala la uwezekano, uonekanaji au hali halisi. Hata kama mambo wanayotaja hayana uhalisia au hayawezekani, kwa sasa ni kitu wanachokitamani kutoka moyoni. Hicho ni kitu fulani. Kwa hiyo ni muhimu kuyawekea majina waziwazi matarajio yao na kuangalia nini ambacho kinaweza kufanyika ili kusogea karibu na kuyafanya mawazo yao kuwa uhalisia.

# 2.11

# DHIMA YANGU KATIKA MAISHA SEHEMU YA 1: KUGUNDUA SHAUKU NA DHIMA KATIKA MAISHA

KARATASI YA ZOEZI 2.11

**Lengo**
Vijana kuchunguza shauku na dhima zao katika maisha.

**Maandalizi**
Rudufisha karatasi ya zoezi 2.11 'Muongozo wa maono ya shauku'. Weka viti katika mduara bila meza. Pembeni mwa darasa panga meza kwa namna ambayo kutakuwa na nafasi ya kufanya mchoro ambao vijana wameuona katika maono yao. Weka tayari karatasi za A3 na rangi mbalimbali za kuchorea katika meza hizo. Hakikisha umetulia na kuwa mpole kabla ya kuanzisha zoezi.

**Maelezo**
'Ili kuweza shauku yako unahitaji kujiangalia mwenyewe ndani yako. Jibu liko katika ufahamu wako. Hapo ndipo utapata jibu kutoka katika moyo wako na namna ya kufanya na njia ya kufuata dhima yako katika maisha. Utaifahamu dhima yako katika maisha utakapoiona. Katika somo hili, utaitambua shauku yako na dhima yako katika maisha kwa maono kupitia kuelezea habari.'

**Utendaji**
1. Waambie vijana wakae katika viti na kuweka miguu yao yote sakafuni.
2. Waagize kuvuta hewa ndani na kutoa hewa nje mara chache, kisha wafumbe macho. Vijana wanaoona kuwa kwao ni changamoto kufumba macho mbele ya kadamnasi wanaweza kuchagua kuelekeza uso wao kwenye kitu fulani sakafuni mbele yao.
3. Waeleze kuwa utawapeleka katika safari fupi kwa kuwaeleza habari ambayo wanaweza kuifuatisha kwa namna yao wenyewe. Chochote kitakachowajia katika akili zao kitakuwa ni chema.
4. Soma ono lifuatalo katika karatasi ya zoezi 2.11 'Muongozo wa maono ya shauku' taratibu na kwa utulivu.
5. Mwishoni mwa maono, waagize vijana kurudi nyuma taratibu kwa muda wanaohitaji. Wahamishe miguu yao na mikono yao na wafumbue macho yao na kuangalia pembeni.
6. Waagize vijana kutawanyika na kukaa katika meza bila kuongea, wakiwa kipande kikubwa cha karatasi (A3) na rangi za kuchorea mbele yao. Waagize waweke katika karatasi kwa maneno au kwa mchoro kile walichokiona katika maono kwa muda usiozidi dakika tano. Wanaweza kutumia picha, maneno, rangi au maumbo mbalimbali. Waandike majina katika karatasi zao.
7. Vijana washirikishane michoro yao na wenzao, waruhusu kuelezea kile ambacho wamekiweka katika karatasi. Labda watahitaji kupiga picha kile walichokifanya kwa kutumia simu zao, kama wanazo.

**Tafakuri**
Pata picha ya jinsi vijana walivyo/wasivyopenda kujiangalia wao wenyewe katika namna hii. Je waliona (vielelezo) vya shauku yao? Waligundua dhima yao katika maisha? Kwa namna gani? Uliza kama vijana wanaweza kushirikishana shauku yao na dhima yao kwa kundi zima.

***Dondoo***

Andaa zoezi kwa kulifanya mwenyewe nyumbani, ili kuona linakupa nini. Mtu mmoja katika kundi anaweza kusoma maono yake kwa sauti. Labda waweza kupenda maandishi yako yawe na mvuto zaidi kwako au kwa kundi lako, waweza kuongeza kitu au kutumia maneno mengine. Jieleze mwenyewe kwa kutumia vifaa vya kuchorea vya rangi mbalimbali. Haina uhusiano na uwezo wako au uwezo wao wa kuchora, picha yako au picha yao ya ndani kwa ulimwengu wa nje. Jipe changamoto mwenyewe na uwape changamoto vijana kufanya matumizi ya kipande chote cha karatasi na vifaa vyote vya kuchorea. Unapogundua na kufuata dhima yako katika maisha, utadhirisha hili katika muonekano mmoja au zaidi:

- haiwezi kukupa njia inayoeleweka ya kile dunia inachotarajia kutoka kwako;
- inabeba hali fulani ya asili ya kutotumia nguvu nyingi;
- inakupa shauku ya furaha;
- kwa mshangao, utajikuta una ujuzi wote unaohitajika kukamilisha dhima yako;
- kuanzia wakati huo, unapoamua kufuata dhima yako, wengine watakufanya uone kuwa umekuwa na msukumo kwao;
- watahitaji kujifunza kutoka kwako na kutaka kujua namna ulivyoweza kufika hapo ulipo;
- utapewa usaidizi wote utakaouhitaji, hata kama ni kwa namna ya kushangaza na ambayo hukuitarajia. Hakuna kitu kama bahati unapojikita kwenye malengo yako, unakutana na watu na mambo yataanza kutokea.

**Uchunguzi wa kina**
Kama nyongeza kwa zoezi hili fanya zoezi la 2.12 'Dhima katika maisha sehemu ya 2: Buni dhima yako'.

2.12

# DHIMA YANGU KATIKA MAISHA SEHEMU YA 2: ANZISHA DHIMA YAKO

KARATASI YA ZOEZI 2.12

**Lengo**
Vijana waanzishe dhima zao katika maisha.

**Maandalizi**
Pangilia chumba chako kwa namna ambayo vijana wanaweza kufanya kazi mmoja mmoja au katika jozi. Chapisha karatasi ya zoezi 2.12 'Dhima yangu katika maisha' kiasi cha kutosha cha nakala kinachohitajika, lakini pia vijana wanaweza kuchora kigae chao. Halafu unahitaji kuwa na karatasi za kutosha na penseli za rangi mbalimbali.

**Maelezo**
'Taasisi yoyote huanzisha dhima kabla ya kuanzisha malengo mahsusi ambayo inataka kufanikisha. Ni jambo jema kufanya jambo hilo pia kama mtu binafsi: Kuanzisha dhima, dhima yako katika maisha. Dhima katika maisha ni wajibu kwako mwenyewe unaoyapatia maisha yako ufahamu wa maana. Umeshafanya zoezi la maono (2.11) ambapo ulitembelea vile vyumba vitatu. Sasa tunaanzisha dhima yetu wenyewe kwa kuanzia hapa tulipo.'

**Utendaji**
1 Agiza kundi lako kufikiri na kujibu maswali yafuatayo mmoja mmoja katika karatasi:
   - Ninafikiria nini juu ya vile ninavyoyapangilia maisha yangu?
   - Naweza kujifunza nini kutokana na hali hiyo?
2 Waruhusu vijana kupata taswira ya majibu yao na waendelee kutokana na kile walichoandika:
   - Nini kinachonipa hisia nzuri?
   - Kipi ninatamani kufanya tofauti?
3 Gawanya kundi katika jozi na ruhusu vijana kujibu maswali na kujadiliana majibu baina yao.
4 Uliza kundi juu ya kiini cha kile walichojadiliana. Lipi wazo la muhimu zaidi la kila mmoja wao? Vijana waweke dhima yao binafsi ya maisha kwenye karatasi, kwa namna ya kigae ambacho kinaweza kuwekwa ukutani au ukurasa wa nje wa kijitabu cha kazi. Mfano wake unaweza kuonekana katika karatasi ya zoezi 2.12 'Dhima yangu katika maisha'.

**Tafakuri**
Shirikisha kundi zima jinsi walivyopitia uzoefu wa taswira yao wenyewe kwa mtindo huu. Uliza vijana kushirikishana kile ambacho wamekiweka katika kigae na kina maana gani kwao.

***Dondoo***

Fanya zoezi hili nyumbani kabla hujalitambulisha katika kundi. Unaweza kuwaeleza kuhusu dhima yako na kuwaonesha namna ulivyolielezea kwenye karatasi katika kigae. Unaweza pia kuchukua hitimisho toka katika zoezi la maono (2.11) katika mtazamo wako, hili litawaonesha vijana namna matokeo yanavyowekwa kwenye muktadha mkubwa zaidi. Watu waliojikita kwenye mambo ya kidini na kiroho watasema kila mtu amepewa dhima katika maisha na kwamba ni wajibu wao kuvumbua dhima hiyo ni ipi. Unapochukua fursa katika maisha ambayo ni kwa ajili yako, utapata msaada usio na masharti toka kwa Cosmos, Allah au Mungu. Watu na namna ya kufanya mambo vitakuja kwa wakati ufaao. Utapitia uzoefu wa kumwagiwa. Utakuwa na uwezo wa kukabidhi kwa mamlaka kubwa zaidi, na hakuna sababu ya kuwa na wasiwasi. Unaweza kuhisi unafanya kitu ambacho kwa hakika ndicho ulichomaanishwa kufanya. Ni wazi kuwa kila hatua au mabadiliko huongeza upeo na dira kwa maisha ya watu wanaoelewa dhima yao katika maisha. Huleta amani kwa sababu hatua na mabadiliko hayo yana maana. Inamaanisha dhima ni muhimu kuliko kazi unayoifanya au unayotamani kuifanya. Dhima katika maisha ni jumla ya vile ulivyo na itakuweka huru kutokana na kile ambacho watu wangekitarajia kutoka kwako. Inaweza kuwa ngumu kutafuta jibu rahisi kwa swali dhima yako nini?

# NGUVU YA KUFANYA KAZI



**Lengo**
Vijana wapitie uzoefu kuwa katika kazi na majukumu mbalimbali kuna vitu ambavyo huathiri kiwango cha nguvu ya utendaji kazi na shauku.

**Maandalizi**
Pangilia viti na meza kwa namna ambayo vijana wanaweza kufanya kazi katika jozi na mmoja mmoja pia. Andika karatasi ya zoezi 2.13 'Nguvu ya kufanya kazi'. Hakikisha una vifaa vya kutosha vya kuwekea alama na gundi ya mikanda.

**Maelezo**
'Wakati mtazamo, matarajio na shauku vinaenda sambamba katika kazi, yawezekana ukafurahia kufanya kazi yako. Mtazamo maana yake ni kwamba kazi yako inatakiwa kuwa na maana, inatakiwa kuwa na lengo la wazi na lenye maana. Kama ufahamu wa mtazamo katika kazi yako, huwezi kutosheka na kile unachokifanya. Unachokiona ni kuwa watu wanapokuwa katika likizo bado wanataka kufanya vitu, siyo kuwa wazembe au kutofanya chochote. Vitu vinahitaji kuleta maana/ufahamu. Utaona kwamba utajisikia vizuri sana wakati kazi yako inapohusishwa na shauku, motisha na vitu unavyovipenda.

Vipi kuhusu wewe, je unafikiria kazi kuwa mzigo, wajibu na jambo unalolipenda au changamoto inayokuongezea nguvu? Kuna kipengele cha tatu ambacho kinaongeza hamu kuhusu kazi. Ni pale ambapo kinashabihiana na kiwango cha uzoefu ulichonacho, uwezo wako, sifa zako na ujuzi wako. Kazi nyepesi haiwezi kukufanya ujivunie, kazi ambayo ni ngumu sana itakufanya kukosa usalama.'

**Utendaji**
1. Waruhusu vijana wafanye utafiti kuhusu kazi zinazohusu utaalamu wao wa baadaye au mafunzo yao ya utendaji ambayo yataanza baadaye kidogo. Inaweza kuwasaidia kufikiria juu ya mtu ambaye tayari anafanya kazi hiyo. Anafanya nini kwa siku anapokuwa kazini. Wanaweza kuorodhesha shughuli zote hizo katika karatasi ya zoezi 2.13 'Nguvu ya kufanya kazi'.
2. Gawa vijana katika jozi, ili waweze kusaidiana na kuongeza orodha ya shughuli ambazo wengine waweza kuwa wameruka.
3. Baada ya hapo kila kijana anafikiria kama vipengele vyote vya kazi ni mzigo, changamoto, wajibu au kitu cha kujifurahisha kwao, na kama vipengele vinahusiana kidogo au kwa wingi na shauku yao. Hata hivyo, vijana wanaweza kutoa majibu tofauti kwa hilo, wanaweza kubadilishana sababu.
4. Vijana wakimaliza, mipango yote inaweza kuwekwa ukutani na wakati wa 'matembezi ya maonesho' wakaribishe vijana kupata taswira za kazi za wenzao na kuulizana maswali.

**Tafakuri**
Uliza vijana wameona nini kuhusu wao wenyewe na kila mmoja wao kuhusu suala la shauku. Ni nini kinacho chochea shauku yao? Ni sehemu gani ya utendaji wao au utaalamu wao wa baadaye ambao vijana waliuangalia? Nini walikiona chepesi, na nini walikiona kigumu? Je wana vidokezo kila mmoja kwa ajili ya mwenzake? Ni kwa namna gani wanaweza kufanya baadhi ya shughuli kuwa na changamoto chache zaidi?

***Dondoo***

Fanya zoezi hili kwa vipengele vya kazi yako mwenyewe. Angalia kama inaoana na kile ulichoking'amua kuhusu kiwango chako cha nguvu ya kiutendaji. Vijana wanaweza kujifunza kutoka katika uzoefu wako.

**Uchunguzi wa kina**
Vijana wapate nafasi ya kuhojiana na mtu ambaye anafanya kazi kama wanayotaka kuifanya kwa siku za baadaye. Vijana waulize mtu huyo kama anapata 'nguvu ya utendaji kazi'. Vijana wanawezaje kusimamia kazi zao au mafunzo yao ili waweze kupata nguvu ya utendaji kutoka katika kazi hiyo? Pendekeza kuuliza kuhusu umuhimu wa baadhi ya shughuli ambazo unapaswa kufanya, au kufikiria namna tofauti ya kutenda baadhi ya kazi.

Hili ni zoezi kubwa sana, inafaa kulifanya mara kadhaa kwa mwaka. Shughuli zilizo ndani ya utaalamu wa baadaye haziwezi kubadilika ndani ya mwaka, lakini vijana wanaweza kujifunza kuwa wataziangalia kazi mbalimbali kwa namna tofauti wakati wanaendelea na mafunzo yao; wanaweza kudhani hazina changamoto kama walivyofikiria mwanzoni. Itakuwa wazi kwao ni kwa njia ipi wanaendelea na kwamba wanapata mafunzo endelevu.

# 2.14

# HABARI YANGU KUHUSU SHAUKU YANGU

**Lengo**
Mwishoni mwa mafunzo vijana watengeneze habari kuhusu matukio muhimu katika miaka (mwaka) ambapo walipata au walikutana na shauku zao.

**Maandalizi**
Weka meza katika namna ambayo vijana wanaweza kufanya kazi (kuandika) mmoja mmoja kuandaa habari zao. Kwa ajili ya uwasilishaji wa habari zao, panga viti katika duara.

**Maelezo**
'Umaizi bila utendaji hauwezi kuleta mabadiliko yoyote. Sasa kwa kuwa umefika mwisho wa mafunzo yako, ni muda wa kuangalia nyuma na kuangalia mbele. Umefanya safari na umepitia uzoefu mwingi sana. Mwingine uliufurahia, na mwingine si sana, mwingine ulikuvutia na mwingine ulikuchosha. Huenda umesahau mengi, kwa sababu hayakustahili kukumbukwa. Na unaweza kuwa na uzoefu wa aina mbili au tatu ambao unaweza kukumbuka maisha yako yote. Katika zoezi hili, utakusanya uzoefu muhimu zaiodi ulioupata katika mwaka/miaka ya mwisho na kuuandikia habari. Si lazima iwe habari nzuri au habari iliyokamilika, lakini iwe habari yako mwenyewe, ambayo tutakwenda kuisikiliza. Tutajifunza kila mtu kutoka kwa mwenzake jinsi ulivyopata uzoefu mwingi katika umaizi, ambao unakuchochea kufanya mambo sawasawa. Hicho ndicho tunaita kujifunza.'

**Utendaji**
1. Agiza vijana kuandaa habari kuhusu shauku yao. Habari isiwe ya zaidi ya dakika 3 na inaweza kusomwa kwa karatasi au kusemwa toka kichwani. Habari pia ianweza kusimuliwa kwa kucheza, ishara, rangi au mchoro. Sisitiza kuwa jambo la msingi ni habari hiyo ni ya maana sana kwa vijana. Inatakiwa ifanane naye, iunganishwe na nguvu zake na shauku yake. Vijana wengine wanatakiwa kuweza kusema kuwa kijana anaiamini habari hiyo. Siyo lazima iwe habari ambayo imeshafanyiwa mazoezi.
2. Vipengele ambavyo habari hiyo inatakiwa kuwa navyo.
   - Kijana anataka kufanya nini baada ya kumaliza elimu yake? Anataka kufanikisha nini?
   - Amefanya nini hadi sasa ili kulikaribia lengo hilo?
   - Je anaweza kutaja mafanikio yake?
   - Anayafikiriaje mafanikio hayo?
   - Hatua zipi ataanza kuzichukua katika siku za usoni?
   - Ana imani chanya zipi juu ya sifa zake mwenyewe?
   - Itakuwaje atakapokuwa amelifikia lengo lake? Atajisikiaje? Watu wanaomzunguka wataelezeaje jinsi alivyofikia lengo?
3. Mpe kila kijana dakika zisizozidi 3 kuelezea habari yake kuhusu shauku yake.
4. Vijana warekodi habari zao kwa kutumia simu zao za mkononi.

**Tafakuri**
Jadili jinsi walivyopata uzoefu kwa kuangalia mafunzo yao na maendeleo yao katika namna hii. Ni kitu gani wanachojivunia zaidi? Nini ambacho wanafikiri walijifunza zaidi? Wanajisikiaje wanapoangalia nyuma kuhusu elimu yao.

***Dondoo***
Wakati vijana wakielezea habari zao, husisha na mawasiliano au maonesho fulani kama: jinsi unavyosimama mbele ya kundi, jinsi ya kuunganisha hadhira yako, ukubwa wa sauti inayosikika, ujasiri unaouonesha, kusema kwa mapumziko mazuri katika maandishi n.k. Toa mrejesho mfupi kwa kila wasilisho na uliza juu ya walau kipengele kimoja muhimu katika wasilisho hilo. Usiwaruhusu kutoa mrejesho wa aina moja kila wakati, waruhusu kuonesha tofauti. Hakuna vidokezo vya kuboresha sasa, ni kukazia tu, jifunze njia hii pia.

# KARATASI YA ZOEZI 2.3

| | | |
|---|---|---|
| Ni nini kilichokugusa sana kwa siku za nyuma? | Je, ni jambo gani zuri sana ambalo mtu aliwahi kukufanyia? | Kumbuka nyakati nzuri sana/nyakati ulipoonja mapenzi makubwa sana. |
| Ni kumbukumbu gani nzuri au ya kufurahisha zaidi kuhusu safari au likizo? | Acha kumbukumbu ya muujiza au tukio la ajabu lijidhihirishe. | Je, una kumbukumbu ambayo una shaka na usahihi wake, lakini hata hivyo bado unaipenda? |
| Fikiria kitu pendwa/ kipande cha nguo/ nyumba/ doa/picha na ulete hadithi ambayo imeunganishwa nayo. | Je, ni kitu gani bora umewahi kuonja, kunusa au kuhisi? | Zikumbuke nyakati ambapo ulifanya uamuzi ambao baadaye umeonesha kuwa wa muhimu sana. |
| Ni nini kilichokufanya ufurahi sana? | Ni nini kumbukumbu yako iliyo laini/ndogo/ pendwa sana/ Kumbukumbu nzuri zaidi? | Je, umewahi kusaidiwa kwa wakati sahihi kabisa? |



# KUTAFUTA HAZINA YA NYAKATI ZA DHAHABU

| | | |
|---|---|---|
| Je, unakumbuka mazungumzo mazuri? | Ni wakati gani mzuri sana leo? | Je, unakumbuka wakati ambao uligundua unayo mamlaka fulani au nguvu? |
| Je, unakumbuka muda ambao uliweza kujisikia kuwa ulikuwa kwenye njia sahihi? | Fikiria wakati ambao ulishiriki katika furaha ya mtu mwingine. | Ni hofu gani ambayo uliishinda kwa kishindo? |
| Je, una siri unayoyajua tu? | Je, unakumbuka wakati ambao ulikuwa umejeruhiwa na asili, au ulijisikia kuungana na asili? | Je, una azma ambayo hakuna mtu mwingine anayejua? |
| Nini ulikuwa ni ufahamu bayana na ufahamu juu ya uponyaji au ugunduzi wako muhimu? | Ni kumbukumbu gani nzuri zinakujia wakati unazitazama dayari ama albamu zako za picha? | Je, ni kumbukumbu gani nzuri zaidi ya kutoa kitu kwa mtu au kufanya kitu kwa mtu? |

# KARATASI YA ZOEZI 2.3

| | | |
|---|---|---|
| Ni kumbukumbu gani ambayo hutaki kupoteza? | Fikiria kumbukumbu ya baadaye ambayo unaweza kuunda sasa hivi. | Fikiria nyuma wakati mzuri wa furaha. |
| Je, ni jambo gani zuri zaidi au kitu ulicho wahi kuona? | Taja wakati ambao ulikuwa na bahati sana. | Tengeneza kumbukumbu ambayo ungependa kuwa nayo au unayoithamini. |
| Umewahi kuwa na furaha ya kipekee siku za nyuma? | Je, umewahi kuwa na uzoefu wa kufanya tukio la ajabu au uvumbuzi wa ajabu? | Kumbuka dhana kubwa ya uzuri. |
| Acha kumbukumbu ya upendo, urafiki au amani ije. | Zikumbuke nyakati za msamaha. | Kumbuka hisia ya siri ya kuridhika ambayo uliyokuwa karibu umeisahau. |



# KUTAFUTA HAZINA YA NYAKATI ZA DHAHABU



| | | |
|---|---|---|
| Acha kumbukumbu nzuri ambayo hujawahi kumshirikisha mtu yeyote kabla ijidhihirishe. | Je, una kovu ambayo unajivunia na huleta kumbukumbu nzuri? | Je, una kumbukumbu nzuri ambayo huleta hisia za furaha? |
| Je, una kumbukumbu nzuri kumhusu nani? | Fikiria kitu ambacho kilikutokea na kwamba wewe tu ndiye unayejua. | Kumbuka wakati ambao ulikuwa umefyozwa (shawishiwa) kabisa na ulifurahia kikamilifu. |
| Fikiria nyuma wakati ulipokuwa umeangaza furaha, ukang'aa na ukaweza kujionesha mwenyewe waziwazi. | Ni harufu gani huleta kumbukumbu nzuri? | Je, unakumbuka wakati ambao ulijivunia sana? |
| Fikiria mtu/kitu ambacho umekikumbuka sana. | Ni lini ulizama sana kwenye mapenzi kwa mara ya kwanza? | Ulishapata ndoto gani ya kustaajabisha/ kushangaza? |

# KARATASI YA ZOEZI 2.5

**A. Mpango wa siku zijazo: shauku yako**

Eleza shauku yako. Unaweza kutaka kuzingatia taaluma au kwenye elimu yako, lakini usiende haraka sana. Unaweza kutaka kutaja matakwa mengine ambayo ni muhimu kwako kwa wakati huu.

**B. Ni nini kinachohitajika kutimiza shauku yako?**

Chunguza nafsi yako ya ndani na tathmini kulingana na mazingira yako; Nini kinakuja akilini mwako?

**C. Nini tayari unacho kwa ajili ya kutimiza shauku yako?**


Jichunguze nafsi yako ya ndani na angalia mazingira yako; Nini kinakuja akilini mwako?

**D. Nini kinakuzuia kutimiza shauku yako?**

Jichunguze nafsi yako ya ndani na kuangalia mazingira yako: Nini kinakuja akilini mwako?

# MANDALA YANGU

MADA YA 2.5



# KARATASI YA ZOEZI 2.6


Barakoa au mkono wako una pande mbili:

**Upande wa nje**, upande unaoonesha ulimwengu wa nje. Hivi ndivyo unavyotaka watu wengine kukuona. Unachofanya kinaweza kuwa cha mfano, tumia ubunifu wako.
**Upande wa ndani**, ndio jinsi unavyohisi, jinsi unavyojiona. Hii pia inaweza kuelezwa kwa mfano, au kutumia rangi zenye maana.

- Chukua karatasi ya (A4) na chora miduara miwili mithili ya yai au vidole viwili.
- Mduara mmoja/alama ya mkono ni upande wako wa ndani, mviringo mwingine/alama ya mkono ni upande wako wa nje.
- Andika maneno (kwenye kipande tofauti cha karatasi) ambacho hukujia akilini mwako wakati unafikiria upande wako wa nje na upande wako wa ndani.
- Kisha nenda kazini; hamisha maneno hayo kwa barakoa/alama yako ya mkono. Tumia vifaa vinavyopatikana. Hivyo ndivyo unavyotengeneza upande wa ndani na nje ya barakoa/alama yako ya mkono.

# BARAKOA YANGU: SEHEMU YA NDANI NA SEHEMU YA NJE

MADA YA 2.6



# KARATASI YA ZOEZI 2.7

Kufanya

Kichwa B

Moyo A

Moyo 1

Kichwa 2

Hisia



# KAULI MBIU YANGU KATIKA MAISHA

MADA YA 2.7

## KAULI MBIU YANGU KATIKA MAISHA

# KARATASI YA ZOEZI 2.9.1

| | | |
|---|---|---|
| **MAHUSIANO YA KIJAMII NA URAFIKI** Ujamaa na kuwa na marafiki wengi mahali pa kazi | **USHIRIKIANO** Kufanya kazi pamoja ili kufikia malengo sawa | **FEDHA** Pata mapato mezuri, sasa na baadaye |
| **UHAKIKA** Kazi imara ambayo ninaweza kuitegemea | **UBUNIFU** Kuwa na uwezo wa kuwa na ubunifu au uvumbuzi | **MASHINDANO** Kuwa na fursa ya kuonesha kuwa nina bora zaidi kuliko mtu mwingine |
| **KUTHAMINI** Kujua kwamba watu wanathamini kile ninachofanya kazi na jinsi ninavyofanya kazi yangu | **SEHEMU YA WAZI** Kuwa na fursa ya kufanya kazi katika eneo la wazi | **UTOFAUTI** Kuwa na utofauti kazini |
| **KUFURAHISHA** Kuwa na wafanyakazi wazuri na mazingira mazuri ya kazi | **MATOKEO YANAYOONEKANA** Kutengeneza vitu, kuwa na uwezo wa kuonesha bayana kazi yangu | **MARA KWA MARA** Kufanya kazi kwa hizo hizo mara kwa mara |





| | | |
|---|---|---|
| **UMUHIMU WA JAMII** Kufanya kazi kwa ajili ya manufaa ya dunia | **JITIHADA ZA KIMWILI** Kufanya kazi ambayo ina changamoto kimwili | **UWAZI** Kufanya kazi katika mazingira ambayo yana sheria na malengo bayana |
| **UHURU** Kuwa na uwezo wa kuandaa kazi yangu kwa njia ninayoipendelea | **UWIANO WA MAISHA – KAZI** Kazi ambayo inaweza kuunganishwa na kutunza familia | **HADHI** Kushikilia nafasi ambayo inaleta heshima katika jamii |
| **KUSAIDIA WATU WENGINE** Kuwa na haja ya watu, kuwasaidia | **KUSAFIRI** Kusafiri sana kwa kazi yangu | **ENEO** Kufanya kazi katika kanda/mkoa maalumu |
| **HATARI** Kuwa na kazi ya kusisimua ambayo sijui nini cha kutarajia | **AMANI** Hakuna misukosuko wala usumbufu | **CHANGAMOTO** Kufanya kazi ambayo inahitaji juhudi nyingi, ina leta changamoto kwenye sifa zangu |

# KARATASI YA ZOEZI 2.9.2

Andika kwa umuhimu wa maadili ya kazi iliyotolewa kwenye kadi 8 ulizochagua.
Andika kwenye safu ya kulia unachomaanisha kwa maadili hayo.

**Maadili muhimu ya kazi yangu:**

1 ______________________

2 ______________________

3 ______________________

4 ______________________

5 ______________________

6 ______________________

7 ______________________

8 ______________________



# MAADILI YA KAZI YANGU



**Nini namaanisha kwa maadili haya:**

**Hitimisho langu:** ______________________

# KARATASI YA ZOEZI 2.10

# KAZI YANGU ILIYO BORA

**Vidokezo kuhusu nini cha kuzingatia wakati unataka kuelezea kazi nzuri unayoitamani.**

**Ungependa kufanya kazi wapi?**

- Ndani ya jengo au nje?
- Daima katika eneo moja au mahali tofauti wakati wote?
- Katika nyumba za watu wengine au katika ofisi?
- Je, ungependa kusafiri kwa ajili ya kazi au ungependa kufanya kazi karibu na nyumbani?
- Katika mazingira ya utulivu au na watu wengi/kelele nyingi karibu yako?
- Je, ungependa kufanya kazi katika kampuni kubwa au katika kampuni ndogo/ yenye ukubwa wa kati?
- Katika kampuni binafsi au ya serikali?
- Katika biashara au mazingira ya kijamii  au yasiyo ya faida?

**Je, ni 'zana' gani utakazofanya kazi nazo?**

- Je, utafanya kazi na 'watu'?
- Je, utafanya kazi na wanyama au mimea?
- Je, unahitaji zana/vifaa kwa kazi yako?
- Je, unafanya kazi/kwa kompyuta au mashine?
- Je, utakuwa na gari la kampuni au utapata fidia ya usafiri wa umma kutoka kampuni?

**Je, utafanya kazi na nani?**

- Peke yako au pamoja na wengine?
- Kufanya kazi zaidi peke yako au zaidi pamoja na wengine?
- Utakuwa na wenzako wangapi?
- Je, utafanya kazi kwa meneja/bosi; Je, utakuwa na biashara yako mwenyewe au utakuwa meneja/bosi wa wengine?
- Je, unakuwa na wateja au wenzako tu ndio pekee utakaoshughulika nao?
- Je, utakuwa unapatikana kwa simu, kwa barua au uso kwa uso tu?
- Je, wenzako watakuwa na umri gani (wastani)?

**Je, hali yako itakuwa katika kazi?**

- Je, utafanya kazi moja kila siku, au utakuwa unafanya kazi tofauti?
- Je, utakuwa unakaa (katika dawati) sana, au utakuwa unatembea na/au utakuwa unasimama sana?
- Je, utakuwa ukiendesha gari au utaenda kwa usafiri wa umma mara nyingi?

# KARATASI YA ZOEZI 2.10



**Je, utakuwa unafanya nini?**

- Je, utafanya kazi kwa mikono yako?
- Je, unafanya kazi na/kwenye kompyuta mara nyingi?
- Je, utakuwa unazungumza na watu/wateja/wagonjwa?
- Je, utakuwa unaandika sana?
- Je, utakuwa na mikutano mingi?
- Je, utahitaji kupanga mambo au kuchukua maamuzi?

**Je, utafanya wakati gani?**

- Wakati wa mchana, jioni, usiku, wakati wa wiki au mwishoni mwa wiki?
- Masaa yasiyo ya kawaida?
- Je, unaweza kujiamulia wakati wa kupanga masaa yako ya kazi?
- Je, utakuwa unafanya kazi wakati wa likizo za shule?
- Ni siku ngapi kwa wiki na masaa mangapi kwa siku utafanya kazi?
- Utakuwa na likizo ngapi kwa mwaka?
- Je, unaweza kuchanganya kazi yako na kuwalea watoto?
- Je, utaweza kuondoa siku moja ya kazi wakati wa harusi au mazishi?

**Je, maneno yako ya ajira/mafao yatakuwa nini?**

- Je, kipato chako kitakuwaje?
- Je, mshahara huo utafanyia nini?
- Kampuni yako hutoa motisha? Lini?
- Je, kutakuwa na matukio ya mwishoni mwa wiki kwa wafanyakazi?
- Je, kutakuwa na matembezi katika kampuni?
- Je, kutakuwa na sanduku la maoni kwa wafanyakazi?
- Je, wafanyakazi watapata fursa ya kufanya mazoezi ya kimwili kwa gharama ya kampuni?
- Je, wafanyakazi hupata fursa ya kufuata kozi/mafunzo/semina kwa gharama ya kampuni?
- Je, kutakuwa na chakula cha jioni kwa wafanyakazi wote?
- Je, huwa unapata fedha za ziada kwa muda wa kazi wa ziada?
- Kampuni huchangia katika mifuko ya kijamii?
- Je, utapata pensheni?

# KARATASI YA ZOEZI 2.11

# MUONGOZO WA MAONO YA SHAUKU

MADA YA 2.11

'Kaa chini, ufuatilie na macho yako yakiwa yamefumbwa. Chukua muda wako kuhisi  jinsi unavyokaa katika kiti chako, wakati makalio yanagusa kiti na nyayo zako zinagusa sakafu. Kisha vuta na kutoa hewa nje, kwa utulivu na wingi. Fikiria uko kwenye ziwa au bahari. Ni mahali pazuri ambapo unajisikia upo nyumbani na umetulia. Unatembea ufukweni. Unaangalia maumbo na rangi zote. Unasikiliza sauti, wanyama, maji, nyayo zako. Unahisi upepo, mionzi ya jua kwenye uso wako. Unakuwa utulivu na kufurahia utulivu na amani ya mahali hapa.

Halafu unaona nyumba. Unapoiona tu, mlango unafunguka wenyewe. Unaichukulia hali hiyo kama ukaribisho. Unaingia ndani ya nyumba. Ndani ya bwalo kuna milango kadhaa. Kila mlango una rangi yake. Unachagua milango mitatu na utaingia katika mlango mmoja baada ya mwingine. Chumba unachoingia kimepambwa kwa rangi kama ile ya mlango ulioingilia. Unapokea ukaribisho na kuangalia hapa na pale na kutafuta kujua dhima yako katika maisha.

Kisha unaona mnyama katika kile chumba cha kwanza. Ni aina gani ya mnyama unamwona? Unamwuliza yule mnyama: 'Chumba hiki kinasemaje kuhusu mimi na je unaweza kuniambia kuhusu dhima yangu katika maisha?' Mnyama yule atakueleza kwanini upo katika chumba hiki na dhima yako ni nini. Anakuambia nini? Unamshukuru yule mnyama na kuendelea katika chumba kingine.
Angalia hapa na pale, unaona rangi nyingine ya chumba na hali hiyo inajirudia tena. Badala ya mnyama unakutana na mtu mwenye hekima, mwanaume mzee mwenye hekima au mwanamke mzee mwenye hekima. Pia, mtu huyu mwenye hekima anakueleza juu ya dhima yako katika maisha au anakuonesha vipengele vyake. Unasikia nini kutoka kwa mtu huyu mwenye hekima. Tena, unamshukuru mtu huyu mwenye hekima na unaendelea kwenye chumba cha tatu. Angalia hapa na pale na utakutana na mtu unayemkubali sana. Ni nani huyu? Unamwuliza tena mtu huyu swali lilelile 'Chumba hiki kinasemaje kuhusu mimi na je unaweza kuniambia kuhusu dhima yangu katika maisha?' Unasikiliza jibu kwa makini.

Sasa, umetembelea vyumba vitatu, unaiacha nyumba hiyo. Chukua majibu ya yule mnyama, yule mtu mwenye hekima na ya yule mtu unayemkubali sana akilini mwako. Kwa mara nyingine unawashukuru na kuwaaga. Kisha unarudi ufukweni mwa ziwa au bahari. Unatembea kidogo na sasa, taratibu, unafumbua macho yako, unapepesa, unajinyoosha na unajua: kila wakati naweza kurudi nyuma.

## DHIMA YANGU KATIKA MAISHA

# KARATASI YA ZOEZI 2.13

Tengeneza orodha ya shughuli tano ambazo ziko katika utaalamu wako wa siku za baadaye au katika mafunzo yako. Labda unaweza kuorodhesha shughuli hizo pembeni, unaweza pia kuzipata kwa kumfikiria mtu anayefanya kazi kama hiyo. Huwa anafanya nini katika siku yake ya kazi?

Fanya tathmini ya kila kazi kwa namna ambayo unaweka sehemu hii ya kazi kuwa na lengo linaloeleweka au lengo lisiloeleweka, kama ni kazi au changamoto, wajibu au jambo la kukufurahisha. Je unadhani shughuli hizi zinachangia kwa kiasi kikubwa au kidogo kwenye shauku yako?

**Kazi ya Tathmini 1**

- ○ Lengo linaloeleweka
- ○ Lengo lisiloeleweka
- ○ Shughuli
- ○ Changamoto
- ○ Wajibu
- ○ Jambo la kufurahisha
- ○ Shauku ndogo
- ○ Shauku kubwa

**Kazi ya Tathmini 2**

- ○ Lengo linaloeleweka
- ○ Lengo lisiloeleweka
- ○ Shughuli
- ○ Changamoto
- ○ Wajibu
- ○ Jambo la kufurahisha
- ○ Shauku ndogo
- ○ Shauku kubwa





**Kazi ya Tathmini 3**

- ○ Lengo linaloeleweka
- ○ Lengo lisiloeleweka
- ○ Shughuli
- ○ Changamoto
- ○ Wajibu
- ○ Jambo la kufurahisha
- ○ Shauku ndogo
- ○ Shauku kubwa

**Kazi ya Tathmini 4**

- ○ Lengo linaloeleweka
- ○ Lengo lisiloeleweka
- ○ Shughuli
- ○ Changamoto
- ○ Wajibu
- ○ Jambo la kufurahisha
- ○ Shauku ndogo
- ○ Shauku kubwa

**Kazi ya Tathmini 5**

- ○ Lengo linaloeleweka
- ○ Lengo lisiloeleweka
- ○ Shughuli
- ○ Changamoto
- ○ Wajibu
- ○ Jambo la kufurahisha
- ○ Shauku ndogo
- ○ Shauku kubwa